# SGR kuwezesha madini, biashara kuinua uchumi mikoa ya Kusini

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOA ya Kusini mwa Tanzania ikiwemo Mtwara na Ruvuma, inakabiliwa na changamoto za kiuchumi na kijamii.

Changamoto hizo ambazo ni pamoja na ukosefu wa miundombinu thabiti ya usafiri na usafirishaji na hata ucheleweshaji wa baadhi ya miradi ya viwanda umesababisha ajira kupungua na biashara ndogondogo kushindwa kukua kwa kasi inayotarajiwa.

Ahadi iliyotolewa katika mkutano wa kampeni uliofanyika Uwanja wa VETA uliopo Songea mkoani Ruvuma mnamo Septemba 22 na mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan anawahakikishia wananchi kwamba, serikali yake itajenga Reli ya Kisasa (SGR) kuunganisha mikoa ya Ruvuma na Mtwara.

Kwa mujibu wa Samia, mradi huu unalenga kurahisisha usafirishaji wa madini kutoka Liganga na Mchuchuma pamoja na kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara za ndani.

**Faida za kiuchumi**

Inaelezwa kuwa, kukamilika kwa mradi huo na hata kuanza kutumika kutasaidia kupunguza gharama za usafirishaji.

SGR inatarajiwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na hivyo, kufanya biashara kuwa rahisi na nafuu.

Faida nyingine za kiuchumi za reli ya kisasa zinazotajwa miongoni mwa nyingi ni pamoja na kuzalisha ajira mpya za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mradi unategemewa kutoa ajira nyingi katika mchakato wa ujenzi, usafirishaji na sekta ya madini na viwanda.

Aidha, utavutia uwekezaji kwa kuwa miundombinu ya kisasa inatarajiwa kuvutia uwekezaji wa ndani na wa kigeni huku wajasiriamali wa ndani wakipata malighafi kwa urahisi na kupanua masoko ya bidhaa wanazozalisha.

**Madini ya Liganga na Mchuchuma**

Mchuchuma kuna makaa ya mawe yenye uwezo wa kuzalisha nishati wakati Liganga kuna madini ya chuma yenye thamani kubwa katika sekta ya viwanda.

Aidha, miradi ya uchimbaji na usindikaji inatarajiwa kuanza rasmi katika Mwaka wa Fedha 2025/26 na kutoa ajira katika sekta ya madini na viwanda.

Mfano wa nchi kutoka Afrika ni

Kenya, ambayo imefanikiwa kuendesha SGR kuunganisha miji ya Mombasa na Nairobi. Matumizi ya reli hiyo yanarahisisha usafirishaji na kuongeza kasi ya biashara za ndani.

Tanzania inaweza kufanikisha mafanikio sawa na hata kwa ubora zaidi kwa kuzingatia bajeti, ratiba na ushirikiano endelevu na sekta binafsi.

Maoni ya wataalamu ni kwamba miradi ya maendeleo kama huo haina budi kupewa kipaumbele kwa kuiondolea vikwazo vya kibiashara na kuchochea ushindani wa kibiashara kwa bidhaa za viwandani ili kukuza uchumi.

"Reli ya Kisasa (SGR) ni hatua muhimu katika kukuza uchumi wa mikoa na taifa kwa ujumla kupitia unafuu na wepesi wa gharama zake katika usafiri na usafirishaji wa bidhaa," anasema Dk John Magafu.

Naye Profesa Martha Qorro anasema: "Miradi hii huondoa vikwazo vya biashara na kuongeza ushindani wa bidhaa za viwandani."

Kwa upande wake, Dk Suleiman Sumra yeye anasema: "Sekta ya madini inapaswa kupewa kipaumbele ili kufanikisha maendeleo ya viwanda."

**Hitimisho**

Mradi wa SGR unaounganisha Mtwara na Ruvuma ni mfano bora wa namna Serikali ya Awamu ya Sita itakavyotekeleza ahadi za Samia.

Utekelezaji unaolengwa, ukishirikiana na maendeleo ya madini ya Liganga na Mchuchuma, utachochea ukuaji wa uchumi, kuunda ajira na kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa wananchi wa Kusini, SGR si tu reli, bali ni daraja la maendeleo, uwekezaji na ustawi wa familia ya kila Mtanzania.

CamScanner

Pg 21

## NISEME NISISEME!

# Usafiri mabasi yaendayo haraka uimarishwe

DAR ES SALAAM

NA DAMAS MAKANGALE

Mfumo wa usafiri wa mabasi yaendayo haraka (BRT) jijini Dar es Salaam, maarufu kama Mwendokasi, ulianza kufanya kazi Mei 10, 2016 (kwa hakika zaidi ni Mei 16, 2016).

Huduma hii muhimu ililenga kuboresha usafirishaji wa abiria (wananchi) kwa wingi, wepesi, haraka na kistaarabu wawahi kufika sehemu za uzalishaji mali; na wanafunzi wawahi shuleni.

Lakini miaka ya karibuni huduma hii imepitia changamoto kubwa. Imegeuka kuwa kero, hasa kwa wakazi wa maeneo ya Dar es Salaam wanaoitegemea; Kimara na Mbezi,

Huduma imegeuka hujuma kwa kuathiri vibaya sana maisha ya raia hawa. Wamekuwa wakichelewa wanakokwenda na wakitaka kuwahi wanalazimika kuingia gharama kubwa!

Msongamano wa abiria vituoni unaosababisha kugombewa kwa mabasi machache yaliyopo kumewasababishia watu majeraha na kuhatarisha maisha yao; huku wazee, wagonjwa na wengine wenye mahitaji maalumu wakishindwa kabisa kuhimili 'ujinga' huo.

Ushahidi wa kero hizi ni picha mjongeo mitandanoni zikionyesha watu walivyojaa na kubanana ndani ya mabasi 30 tu eti ya kuhudumia watu 200,000 kwa siku, kiasi hata cha kushindwa kufunga milango.

Ukweli ni kwamba ni vigumu sana kuendesha huduma ya mwendokasi kwa kutegemea kupata faida ya kibiashara (as a profitable business).

Pasi na shaka mfumo wa kitaifa kama mwendokasi unahitaji uwekezaji ambao hauwezi kulipwa kwa tiketi pekee.

Mifumo kama BRT, Tram, Metro na hata SGR haijengwi kwa malengo ya faida ya moja kwa moja, bali kwa faida pana za kijamii, kiuchumi na kisiasa kama kupunguza msongamano, kuokoa muda, kuongeza tija, kusaidia usawa wa kijamii, kuimarisha hadhi ya taifa na hata kulinda mazingira kwa kupunguza matumizi ya magari binafsi iwapo huduma ni fanisi.

Kwa mizania hiyo nchi nyingi zilizoendelea duniani huwekeza na kutoa ruzuku kuhakikisha mifumo inafanya kazi na si kuendeshwa kwa malengo ya kupata faida.

Hii ni huduma ya kijamii na muhimu kwa serikali kuwekeza zaidi na kufungua milango ya kutoa ruzuku!

Kwa hiyo ni muhimu kwa serikali kulitazama kwa jicho la kipekee suala hili. Kwamba hii ni huduma ya kijamii si sehemu ya kupata mapato na faida kama biashara nyingine.

Kwa msingi huo, ni lazima serikali iweke malengo ya kutanua uwekezaji wa mwendokasi ili kuongeza tija kwa usafiri wa umma nchini.

Pamoja na mambo mengine, ni muhimu kupata fursa ya hasa watendaji wakuu wa huduma hii kwenda kujifunza ng'ambo jinsi huduma hizi zinavyoendeshwa kwa tija na kwa ufanisi.

Serikali iwekeze na kutoa ruzuku ili uwekezaji huo uwe na tija kwa masilahi mapana ya nch yetu.

Ni vema tukaipongeza serikali kwa kuchukua hatua stahiki kufuatia kilio cha wananchi na kuamua kuleta mabasi mapya ili kupunguza adha ya usafiri iliyopitiwa na wakazi wa Kimara na Mbezi.

Pongezi hizi za serikali na taasisi zake za kuongeza mabasi kwa ajili ya abiria na wananchi kwa ujumla inabidi ziende sambamba na umuhimu wa Watanzania kujua kwamba ni jukumu lao pia kutunza mabasi haya ya umma.

Watanzania wafahamu kuwa hii ni mali yao, waheshimu maelekezo na miongozo iliyopo. Viti vilivyotengwa kwa walemavu, wazee na wajawazito viachwe kwa ajili yao.

Watanzania wajue kwamba si uungwana kuharibu mali ya umma. Ni uhujumu uchumi.

Kilichotokea wiki iliyopita Gerezani, Magomeni na Kimara kwa wananchi (abiria) kupiga mawe na kuharibu mabasi haya ya umma si cha kiungwana na kinapaswa kulaaniwa.

Ni haki ya raia kudai huduma bora za usafiri, lakini haki hii idaiwe kwa njia ya amani na serikali itasikiliza!

Ndiyo maana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alikwenda Kimara na kujionea mwenyewe adha ya usafiri. Hatua ikachukuliwa, mabasi ya Mbagala sasa yanafanya kazi Kimara.

Naam! Pamoja na mambo mengine, Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko ya uongozi wa mwendokasi.

Kilichobaki ni kwa serikali kutambua kuwa uwekezaji na ruzuku ni mambo muhimu ili kuhakikisha huduma hii ya kijamii inaendelea kuwapo kwa ufanisi wa kutosha kwa masilahi ya Watanzania wote, huku ikiendelea kulinda usawa wa kijamii, mazingira na miundombinu iliyoboreka na wenye kufungua fursa za kiuchumi, kibiashara na kijamii.

**dkangale1@gmail.com**
**0658-306838**

Nipashe Jumanne Oktoba 7, 2025 Pg 19

# Nchimbi asema SGR ni injini ya uchumi mpya

**Na Gwamaka Alipipi,**
TABORA

MGOMBEA Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ni mradi wa kimkakati ambao utageuza sura ya uchumi wa Tanzania na ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Kibwe B, Jimbo la Igalula mkoani Tabora, Dk. Nchimbi alisisitiza kuwa reli hiyo si mrundikano wa chuma na saruji, bali ni uti wa mgongo wa uchumi wa baadaye wa taifa.

"SGR ni zaidi ya reli - ni daraja la maendeleo. Kutoka Makutopora hadi Kigoma, reli hii itaunganisha Watanzania wa mijini na vijijini, kufungua masoko mapya na kupunguza gharama za usafirishaji kwa kiwango kikubwa," alisema.

Akiwa katika kampeni za CCM kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, Dk. Nchimbi alieleza kuwa mradi wa SGR utaharakisha ukuaji uchumi, kukuza ajira na kubadili maisha ya mamilioni ya Watanzania.

SGR inapita Wilaya ya Uyui na Jimbo la Igalula kupitia vipande muhimu vya ujenzi vinavyoweka Tabora kuwa kiungo kikuu cha usafiri: Makutopora-Tabora (Km 368), Tabora-Isaka (Km 165), Mwanza-Isaka (Km 341), Tabora-Kigoma (Km 508), na Uvinza-Musongati (Km 282).

Alisema reli hiyo itapunguza muda wa usafirishaji mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda nchi jirani kama Rwanda, Burundi na DRC, huku pia ikipunguza msongamano wa magari barabarani na gharama za biashara.

"SGR si tu itabeba mizigo, bali itabeba ndoto za vijana wanaotafuta ajira, wakulima wanaotafuta masoko na wafanyabiashara wanaotafuta faida," alisema Dk. Nchimbi.

Alieleza kuwa maelfu ya ajira zimekwishaibuliwa na nyingine zitaendelea kupatikana kupitia shughuli zinazohusiana na ujenzi na uendeshaji wa reli hiyo.

Vilevile, aliahidi kwamba serikali ya CCM itaendelea kuwekeza katika maeneo ya viwanda, vituo vya usafirishaji mizigo, na biashara ndogo kuzunguka vituo vya reli.

Katika sekta ya kilimo, Dk. Nchimbi alitangaza mpango wa ujenzi wa bwawa jipya la umwagiliaji katika Igalula pamoja na kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji pembejeo za kisasa.

Alisema miradi hiyo itaungwa mkono na kuwapo reli ya SGR kwa kurahisisha usafirishaji mazao kwenda kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi.

Pia alisisitiza kuwa maeneo mengi ya vijijini yanatarajiwa kufikiwa na huduma za umeme kupitia miradi ya REA, ili kuchochea kilimo cha kisasa na shughuli nyingine za kiuchumi.

Kwa upande wa biashara za kikanda, Dk. Nchimbi alisema Tanzania chini ya CCM itaendelea kujenga mazingira rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara, huku SGR ikiwa msingi wa ushindani katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"SGR ni nyenzo ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara kwa Afrika Mashariki na Kati. Itapanua masoko, kuongeza ushindani na kurahisisha biashara ndani na nje ya mipaka yetu," alisisitiza.

"SGR ni injini ya fursa. Ni urithi wa vizazi vijavyo. Ni ahadi ya CCM kwa maendeleo ya kweli, yenye kugusa maisha ya watu," alisema.

CamScanner

UTENDAJI

# Dk Dau: Hii ndiyo Udart tuitakayo

Dk Ramadhani Dau

**Dar es Salaam.** Ilikuwa siku ya Alhamisi, Oktoba 2, 2025, wakati natoka kuswali swala ya Alasiri katika Msikiti wa Mjimwema, Kigamboni, nilipopigiwa simu na mmoja kati ya watu wangu wa karibu kuniarifu kuwa nimeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Usafiri Dar es Salaam (Udart).

Baada ya simu hiyo, nilianza kupokea salamu za pongezi na za pole kwa simu na ujumbe wa WhatsApp kutoka kwa watu mbalimbali, mmoja mmoja na kutoka makundi sogozi mbalimbali.

Kwa hakika, malalamiko yalikuwa mengi. Si nia yangu kuyaorodhesha hapa, kwani kufanya hivyo itakuwa sawa na kukosha nguo zako chafu hadharani.

Lakini kwa ujumla wake, mengi yalikuwa katika maeneo ya huduma mbaya kwa wateja, hujuma kama vile mabasi kwenda matupu na kuwaacha abiria vituoni kwa kisingizio kuwa muda wa kazi wa dereva umemalizika, abiria kutorudishiwa "chenji" zao wakati wa kulipa nauli, ubadhirifu wa mali, na mengine mengi.

Baada ya utangulizi huo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema.

Pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais, Dk Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mwenyekiti wa Kampuni ya Udart, hasa ikizingatiwa changamoto zilizojitokeza hivi karibuni. Hii ni dhamana kubwa kutokana na unyeti wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mimi na wenzangu kwenye Bodi na Menejimenti tutafanya kila liwezekanalo, ambalo lipo ndani ya uwezo wa kibinadamu, kutimiza wajibu wetu, kwani Kanuni ya Fiqh inatuelekeza kuwa, "lisilowezekana lote, lisiachwe lote."

Nikiri kuwa hii si mara yangu ya kwanza kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tofauti na teuzi zote nilizopita, kwenye uteuzi huu nimepata salamu nyingi sana. Pamoja na pongezi, wengi wao walinipa pole.

Yupo ndugu yangu mmoja ambaye ni sahiba wangu wa miaka mingi aliniambia kuwa hatonipa pongezi mpaka aone mabadiliko makubwa kwenye usafiri wa Dar es Salaam. Alikuwa sahihi kabisa. Nawashukuru wote kwa salamu zenu.

Kufuatia changamoto zilizopo kwenye Udart, niliamua kufanya ziara ya kimya kimya kwa kupanda basi kama abiria wa kawaida, ili nisome na kuielewa vyema Udart. Nafahamu kuwa ziara ya siku moja haitoshi kuielewa vyema taasisi yoyote, lakini nilidhani ziara hiyo itanipa utambulisho (introduction) mzuri wa Udart.

Sharti ambalo mimi mwenyewe nilijiwekea ni kuwa, katika ziara hiyo, nisingependa watu wanitambue, kwani nilitaka niyashuhudie mambo katika uhalisia wake.

Kabla ya kufanya ziara hiyo, nilitaka ushauri kutoka kwa watu mbalimbali huku nikiwaeleza sharti langu. Katika kuficha kujulikana (identity) kwangu, nilifikiria nivae mavazi ya kawaida, lakini nivae kofia ambayo maarufu inajulikana kama kapelo.

Baada ya kuwaeleza dhamira yangu, mmoja kati ya dada zangu (jina ninalihifadhi) ambaye ana wadhifa mkubwa serikalini, alinishauri kuwa kama kweli nataka nisijulikane, ni vyema nikavaa buibui na ikiwezekana nifunike uso wote isipokuwa macho tu.

**Oktoba 2**

Siku ambayo Rais Samia Suluhu Hassan alimteua Balozi Dk Ramadhani Dau kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART).

**Oktoba 5**

Siku ambayo Dk Dau alifanya ziara ya kimya kimya kwa kupanda usafiri wa mabasi hayo kama abiria wa kawaida.

Uvaaji huu maarufu unajulikana kama ninja. Dada yangu alinishauri kuwa, kinyume cha hivyo watu watanifahamu na dhamira yangu haitotimia.

Baada ya kupokea ushauri huo, nikajadiliana na mke wangu kwa sababu mbili. Kwanza, mimi sina buibui, hivyo basi, itabidi niombe la kwake, hasa kwa vile vimo vyetu havipishani sana. Pili, ni vyema jambo kubwa kama hilo la kubadili mavazi ningepata ushauri na ridhaa yake.

Wazo hilo likaonekana si zuri kwa sababu, kwanza, hairuhusiwi kuvaa ninja kwenye mwendokasi; lakini pili, endapo atatokea mtu akanitambua, itakuwa fedheha kubwa kwangu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Udart, Balozi Dk Ramadhani Dau akiwa ndani basi la mwendokasi alipofanya ziara ya kimya kimya.

Kwa maana hiyo, niliamua kuvaa nguo za kawaida na kofia ya kapelo. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana, wakati naondoka nyumbani nilisahau kofia yangu.

Nilianza ziara Jumapili, Oktoba 5, 2025, saa 5:50 asubuhi, katika Kituo cha Posta ya Zamani kuelekea Kimara, ambapo tulifika saa 6:20.

Nilikaa Kimara kwa takribani dakika 15 na kuondoka saa 6:35, na kufika Posta ya Zamani saa 7:10. Wakati wa kwenda, sikubahatika kupata kiti, nilisimama kutoka Posta ya Zamani hadi Kimara. Kwa bahati, wakati wa kurudi nilipata kiti kutoka Kimara hadi mwisho wa safari yangu.

Kwenye safari yangu yote (kwenda na kurudi), nilipata bahati mbaya ya kupanda mabasi mapya yenye rangi ya kijani iliyokolea.

Nasema ilikuwa bahati mbaya si kwa sababu ya rangi ya mabasi au sababu nyingine yoyote, isipokuwa nilitamani kupanda mabasi ya zamani yenye rangi ya buluu ili nifanye tathmini ya hali ya mabasi hayo, ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kuwa ni mabovu. Natumai Balozi Hamza atanielewa.

Katika ziara hii, nimejifunza mengi sana. Mengi ya malalamiko niliyoambiwa, nimeyashuhudia. Hata hivyo, hapa si mahali pake.

Ni mambo ambayo tutajadiliana kwenye vikao vya Bodi na Menejimenti, ili tupate ufumbuzi wa matatizo hayo. Tutajitahidi kuwajuza wananchi jitihada zinazofanywa kuondoa kero hizo.

Kwa bahati nzuri, ile dhamira yangu ya kutotambuliwa ilitimia, isipokuwa wakati wa kurudi. Tulipofika Manzese, kuna kijana mmoja alinikaribia na kunitazama kwa muda mrefu kidogo.

Baada ya macho yetu kukutana, aliniamkia, nami nikaitikia. Kwa sababu nilikuwa nimekaa, haraka nikatoa simu yangu na kuanza ku-chat ili kukwepa asianze kunisemesha na kuwafanya watu wengine wanitambue. Kwa kumalizia, naomba niwakumbushe wakurugenzi wenzangu na menejimenti kuwa dhamana tuliyopewa ni kubwa, na matarajio ya wananchi ni makubwa.

Nina imani tukifanyakazi kwa juhudi, maarifa, ikiwemo ubunifu na kuweka uzalendo mbele, tutatoa mchango mkubwa kwa nchi yetu.

Kwa wafanyakazi wa Udart, naomba mkae mguu sawa, kazi ya kujenga Udart mpya imeanza!

*Mwandishi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Udart.*

CamScanner